

MLANGO WA KUINGIA MOYONI

 ...nguo na lesu, na akawaomba wahudumu wote waje huku, na wapendwa, ili tuweze kuweka mikono yetu juu ya vitambaa hivi, na kumwomba Mungu asaidie.

² Baba wa Mbinguni, kanisa hili, kwa moyo mmoja, wanakuja Kwako, wakiomba lesu hizi zipakwe mafuta kwa Roho Mtakatifu, ili vitakapoenda kuwekwa juu ya wagonjwa na wanaoteseka, kila mmoja na aponywe. Tunapoomba kwa moyo mmoja tukiomba rehema ya Kiungu ya Mungu kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka, kulingana na Maandiko na utajiri wa Yesu Kristo na neema Yake. Tunaomba, katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

³ Asante, ndugu. Asante, ndugu. Mnaweza kuketi. Asanteni.

⁴ Haya yamekuwa majuma mawili mafupi sana kwangu, na nikijua ya kwamba kesho inamalizia mkutano huu. Nilikuwa tu nikimwambia Ndugu Shores, jinsi ninavyothamini ushirikiano wake mzuri. Na Ndugu...ndugu wote, na dada wote, na wote walioingia, Four Square, Church of God, Jina la Yesu, Maskani ya Imani, na hayo yote, Assemblies, na kila mtu, hakika tunathamini ushirikiano wenu.

⁵ Na sasa kesho, kama kuna wageni hapa, sasa, ninawatakeni myatafute makanisa haya ambapo ninyi, kanisa lenu wenyewe la dhehebu lenu wenyewe na mwende huko, kanisa ulilochagua, popote unapotaka kwenda, kutakuwako na ibada katika hayo yote kesho. Na sasa, hatuninii...sisi—sisi hapa tu, kwa namna fulani, tunaingia namna hii, na, kutembelea.

⁶ Na, bila shaka, sisi, kama huna kanisa, tungefurahi kuwa pamoja nawe kesho usiku. Lakini kama kanisa lako lina ibada kesho usiku, huo ni wajibu wako, hapo ndipo mahali pako pa wajibu kanisani mwako. Kamwe hatutaki mtu yeyote kuliepa kanisa lao wenyewe. Kamwe hatutaki mtu yeyote kuchukua pesa kama wangeziweka kanisani mwao wenyewe, kudhamini mmoja wa mikutano hii. La, bwana. Kwamba...Zaka yako na matoleo yako yanaingia katika kanisa lako mwenyewe.

⁷ Kama unajisikia kusaidia katika mmoja wa mikutano hii, ama kitu fulani, baada ya kanisa lako mwenyewe kushughulikiwa, hilo ni sawa. Lakini hatutaki kamwe kuchukua senti moja kutoka kwa kanisa lolote, tunajaribu kulisaidia kanisa hilo, tunajaribu kufanya yote tuwezayo ili kwamba uwe mfuasi bora zaidi wa kanisa hilo. Haidhuru ni kanisa gani, tunataka uwe mfuasi mwaminifu kwelikweli, na umtumikie Bwana Yesu kwa moyo wako wote.

⁸ Sasa, halafu kesho usiku ni ibada ya kumalizia na...Je, mlipenda ibada ya uponyaji ya jana usiku? Hiyo ilikuwa...?

Unapenda ninii ya namna hiyo...? Vema, mngetaka kuwa na nyingine kesho usiku namna gani? Hilo lingekuwa sawa? Vema, basi nitawaagiza wagawe kadi za maombi tena kesho usiku yapata saa kumi na mbili, kama kawaida, ama wakati wowote wao... Ni kitu gani, yapata saa kumi na mbili ama...? Saa kumi na mbili, sawa, saa kumi na mbili. Sawa, saa kumi na mbili. Na kwa hiyo, watakuwa hapa kugawa kadi za maombi kesho usiku. Nasi tutawaombea wagonjwa tena kesho usiku katika—katika mstari wa maombi.

⁹ Mtu yeyote anaweza kuzipata, hazina—hazina gharama, hazikugharimu hata senti moja, wewe njoo tu, haziuzwi. Hiyo ndiyo sababu nimemweka mwanangu mwenyewe kuzigawa. Ili kusiwe na gha—gharama yoyote kamwe kwazo, kusiwe na upendeleo... tunazigawa tu. Mtu yeyote anayezitaka, zichukue tu. Wakati mwingine wakati tunapokuwa na...

¹⁰ Tena ninamwomba pia, kwamba wakati tunapokuwa na mistari ambapo inatubidi kuwaita tu wachache, mimi humwomba asimame mbele ya kusanyiko, na kuchanganya kadi hizo zote pamoja, kisha azigawe tu. Kwa sababu hakuna mtu... Naye... Na ili kulihakikisha maradufu, hakuna ajuaye mahali mstari wa maombi utakapoanzia katika mkutano huo. Hata mimi mwenyewe sijui, huo ndio ukweli. Ninasimama hapa, na mahali ambapo Bwana anaweka moyoni mwangu kuanzia, hapo ndipo ninapoanzia.

¹¹ Nilizoea kumwita mtoto mdogo aje ahesabu, na popote angesimama, ningeanzia hapo. Hilo halikufanya kazi vizuri sana, mwajua, mama alimfanya Kadogo kusimamia mahali ambapo namba yake ilikuwa. Kwa hiyo, tungali tunashughulika na wanadamu. Lilikuwa ni la kupendeza, bali halikuwa sawa tu kwa watu.

¹² Na kwa hiyo, ndipo tunashuka, mwanzoni mwa mkutano tungegawa kadi zote za maombi. Hiyo ni wakati walipokuwa na mikutano mikubwa, na labda zikasambazwa kwa mamia. Vema basi, mimi... Hakuna haja ya mtu yeyote kuja baada ya usiku huo wa kwanza. Kama tungekuwa huko majuma mawili, nisingewapitia hao wote, yapata watu sita ama wanane kwa usiku mmoja, kumi, mnaona, kamwe nisingeweza kuwamaliza, kwa hiyo hilo halikufanya kazi. Watu, kama hawakuwapo huko siku ya kwanza hawakuwa na nafasi ya kuingia kwenye mstari wa maombi.

¹³ Kwa njia hii, kila mtu huja. Kila mtu ana ninii sawa... Nasi tunajaribu sasa kupitia tu mstarini, tunaliombea kundi zima, na mtu yeyote anayetaka kuombewa, nafikiri hilo ndilo bora zaidi tuwezalo kufanya. Kuelezea imani, kwamba imani yako ndiyo inayokuponya.

¹⁴ Sasa nataka kusoma usiku wa leo, kama mnayafuatilia Maandiko, ninataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Ufunuo

wa Yesu Kristo, ambacho hivyo ndivyo kilivyo. Ufunuo wa Yesu Kristo mlango wa 3. Bwana alibariki Neno Lake. Nasi tunataka kusoma juu ya hali ya kanisa la siku hizi, Wakati wa Kanisa la Laodikia. Tukianza na kifungu cha 14:

...kwa malaika wa kanisa lililoko...Laodikia andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina, shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu;

Nayajua matendo yako,...hu baridi wala hu moto: ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto.

Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu.

Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha,...sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge,...mwenye mashaka,...maskini,...kipofu, na uchi:

Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa...moto, upate kuwa tajiri; na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.

Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi: basi uwe na bidii, ukatubu.

Tazama, nasimama mlangoni, nabisha: mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, Nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.

Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda, nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.

Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.

¹⁵ Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno.

¹⁶ Na sasa, msisahau, ombeni. Tulikuwa tukiimba wimbo mdogo kanisani mwetu. Sijui kama mnauimba hapa au la. Nisingeweza kuimba, sikuzote nilitaka kuimba. Lakini ni—nilifikiri ningejaribu, lakini ujasiri wangu hautaniruhusu kufanya hivyo. Nitasema tu:

Ombeni, ombeni, ndiyo njia pekee

Kufikia mahali pa juu;

Ombeni, ombeni, maombi ya imani

Yatashusha baraka za Mungu.

Hiyo ni kweli.

¹⁷ Ni wangapi wanaopenda uimbaji mzuri? Loo, hilo ni sawa. Ninaupenda tu. Nilimsikia huyu Ndugu Mushegan hapa asubuhi ya leo akiimba kule chini kwenye kiamshakinywa. Na ni wakati

mzuri jinsi gani tuliokuwa nao! Ninapenda tu uimbaji na uimbaji wa kiroho. Ninapenda uimbaji mzuri wa kale, wa Kipentekoste, kuimba katika Roho. Ninachukia kusikia sauti iliyofunzwa kupita kiasi. Hmm! Wakishikilia pumzi yao mpaka wanageuka bluu usoni na hawajui kile. . . Wanaimba tu wapate, kusikika. Lakini napenda tu uimbaji mzuri, wa mtindo wa kale, wa Kipentekoste ambapo tu wanapiga makofi na kuwa na wakati mzuri. Huo ni uimbaji mzuri. Sikuzote nilitaka kuimba wimbo huo:

Neema ya ajabu! Jinsi inavyosikika tamu,
 Iliyomwoko mwovu kama mimi!
 Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa
 nimepatikana,
 Nilikuwa kipofu, lakini sasa ninaona.

¹⁸ Si—sina sauti ya kuimba. Lakini siku moja wakati nyote mtakapofika Ng'ambo ya pili, nanyi mnaishi katika jumba lenu kubwa huko juu mahali fulani, mkimtukuza tu Mungu, huko chini kabisa mwituni kuna kibanda kidogo, kilicho pale chini pembeni. Nawe utakapotokea kwenye ukumbi wako wa mbele asubuhi moja, utamwona mtu amesimama pale kibandani, utasikia sauti ikitoka mwituni ikiimba, “Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika tamu, ilimwoko mwovu kama mimi.”

¹⁹ Useme, “Mungu asifiwe, maskini Ndugu Branham alifaulu, huyo hapo, anaweza kuuimba sasa.” Hatimaye alifaulu, akafika Ng'ambo ya pili.”

²⁰ Na kama. . . Njia pekee nitakayoweza kufika kule ni kwa neema ya ajabu ya Yesu Kristo. Ninapenda, ninamtumaini, bali itahitaji neema Yake kunifikisha Ng'ambo ya pili. Kwa hiyo, situmainii uwezo wowote, sina, ninatumainia yale aliyonifanyia.

²¹ Yeye ni Mpatanishi wangu, Yeye ni Upatanisho wangu kwa ajili ya dhambi zangu, Yeye ni Maji ya farakano, Yeye ni Alfa, Omega, Yeye ni Uzima wangu, Kuzaliwa kwangu, Baba yangu, Mama yangu, Dada yangu, Ndugu yangu, Bwana wangu, Mfalme wangu, Mwokozi wangu, Mponyaji wangu, Yeye ni Yote katika Yote kwangu.

²² Nawapenda ndugu zangu, nawapenda dada zangu, lakini, loo, huo upendo wa fileo kamwe usingepachukua mahali pa huo upendo wa Agapao wa Roho Mtakatifu. Ninapenda mke wangu, watoto wangu kama tu vile mume au baba yeyote angeweza, bali kamwe hautagusa mahali hapo patakatifu pa huo:

Upendo wa Mungu, jinsi ulivyo mwingi na safi!
 Jinsi usivyopimika na wenye nguvu!
 Utadumu milele,
 Wimbo wa watakatifu na wa malaika.

²³ Loo, ninaupenda huo! Afadhali nisimame sasa.

²⁴ Katika kifungu cha 20 cha mlango huu fulani wa Ufunuo hapa, mlango wa 3 na kifungu cha 20, ninataka kusoma fungu, kama ningeliita hivyo, nizungumze kwa muda kidogo, kisha tuone yale Baba yetu wa Mbinguni atatutaka tufanye, sijui.

Tazama, nasimama mlangoni, nabisha: mtu akiisikia sauti yangu, na kufungua mlango, nitaingia kwake, nami. . . nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.

²⁵ Unasema, “Ndugu Branham, hilo ni fungu dogo sana kwa umati wa watu wa ukubwa huu.”

²⁶ Lakini mnajua, si ukubwa wa maandishi, ni yale yaliyomo ndani yake. Kuna ya kutosha mle ndani kuyafungua macho ya kila mwenye dhambi ulimwenguni, kuna ya kutosha mle ndani kuuokoa ulimwengu mzima. Mnajua, mambo siku hizi, tunaangalia mambo makubwa, lakini tunaacha mambo madogo.

²⁷ Hapa wakati fulani uliopita, sijui kama nimewahi kuwaambia habari zake ama la, ilikuwa ni katika mji fulani, mvulana mdogo alikuwa darini akiangalia kote, ndipo a— akapata kwenye kasha la kale stempu ndogo ya posta, yapata tu nusu inchi mraba. Vema, alijua mahali palipokuwa na mkusanya stempu huko chini mtaani, kwa hiyo akakimbia mtaani, alidhani labda huyo mkusanya stempu angempa senti tano kwa ajili ya hiyo stempu ya posta akaiweke kwenye albamu yake, nayo ingeninii. . . angejinunulia koni ya aiskrimu.

²⁸ Basi akashuka mbio mtaani kwa mkusanya stempu, naye akasema, “Angalia stempu hii niliyoipata sasa hivi,” naye akamwita kwa jina lake alilopewa. Kasema, “Utanipa kiasi gani kwake?”

²⁹ Naye mkusanya stempu akaiangalia kwa darubini yake, ilikuwa ni kuukuu na imegeuka manjano, akasema, “Loo, ni— nitakupa dola moja kwake.”

³⁰ Loo, mapatano yakafanywa upesi sana, na biashara ilikuwa inaendelea. Hizo zilikuwa ni kama koni ishirini za aiskrimu. Loo, akauza hiyo stempu upesi sana. Huenda nimekadiria juu ama chini, lakini ninaamini stempu hiyo iliuzwa yapata majuma mawili baadaye kwa karibu dola mia tano. Halafu baadaye, ikauzwa kwa kiasi kikubwa mno, na imeendelea kupanda zaidi na zaidi, mpaka sijui hiyo stempu ina thamani gani. Ni mojawapo ya stempu zenye thamani zaidi zilizopo kwenye albamu ya mkusanyaji. Ni kitu gani kilichoifanya kuwa ghali hivi? Haikuwa kwa sababu ya ukubwa wake, haikuwa kwa sababu ya karatasi iliyokuwa imeandikiwa, kwa sababu tayari ilikuwa imegeuka manjano, bali kilichokuwa juu yake ndicho kilichojalisha.

³¹ Hivyo ndivyo ilivyo kwa fungu hili usiku wa leo ama Andiko lolote. Si ukubwa wake, wala karatasi liliyoandikiwa, ni yale yaliyoandikwa juu yake. Ni Neno la Mungu aliye hai, ambalo ni la Milele tu sawasawa na Mwandishi wa hayo Maandiko, kubwa,

na kila ahadi ni kweli. Si ya kawaida, pia, kwa sababu inaleta picha ya mtu akibisha mlangoni.

³² Siwezi kabisa wakati huu kutaja jina la msanii aliyeandika picha hiyo maarufu, ama aliyeichora, hasa, aliyeipaka rangi. Kwamba alisimama na kuchora picha ya Yesu akiya na kubisha mlangoni. . . Nafikiri alikuwa ni msanii wa Kiyunani, hakuwa 'Angelo, sidhani, bali sina hakika jina lake lilikuwa ni nani. Lakini picha zote maarufu, kabla hazijapata umaarufu, hazina budi kupitia kwenye ukumbi wa wakosoaji.

³³ Mara nyingi nimewazia hilo kuhusu Kanisa. Kabla Mungu hajaweza kulichukua Kanisa Lake katika Unyakuo, halina budi kupitia kwenye ukumbi wa wakosoaji, walimwengu, kulikoso, kulidhihaki, kuliita jina lingine.

³⁴ Lakini basi, wakati hatimaye imepitishwa kwenye ukumbi huo wa wakosoaji, basi hiyo picha au huo mchoro unaweza kutundikwa kwenye ukumbi wa umaarufu. Hivyo ndivyo Mungu atakavyofanya na Kanisa Lake, Yeye ataliacha lipitie ukosoaji na mateso ya ulimwengu, lakini siku moja Yeye atalipeleka juu hewani na kuliweka kwenye ukumbi wa umaarufu, na kuliketisha mkono Wake wa kuume.

³⁵ Huyu msanii mashuhuri, ilikuwa imemchukua maisha yake yote kuichora hiyo picha. Wakati, hatimaye, alifikiri yote yalikuwa tayari kwa ajili ya ukumbi wa wakosoaji, ndipo baada ya kitambo kidogo mkosoaji fulani akatokea, nao wameelimishwa kukoso, wakosoaji wakuu maarufu, naye akasema, "Picha yako ni picha nzuri sana. Tunaweza kumwona nanii, Yesu akiya usiku katika giza la maisha ya mwanadamu akiwa na taa yake mkononi, tunaona maskini makazi mazuri, anayokujia, na mizabibu karibu na mlango, na kadhalika, tunamwona akiwa na sura kama hiyo usoni mwake, akibisha, akisikiliza, akijaribu kusikia kama kungekuwa na jibu kutoka mle ndani."

³⁶ Yule mkosoaji akasema, "Hakuna kitu cha kukoso hiyo, umefanya kazi nzuri sana. Ila kuna jambo moja tu ambalo umeshindwa kufanya."

Ndipo huyo msanii akasema, "Bwana, ni jambo gani hilo ambalo nimeshindwa kufanya?"

Akasema, "Umeshindwa kuweka komeo mlangoni." Kasema, "Hakuna komeo juu yake."

"Loo," kasema huyo msanii, "niliichora hivyo."

Vema, akasema, "Yeye angewezaje kuingia kama hakukuwako na komeo?"

Akasema, "Komeo liko upande wa ndani. Mtu aliye ndani hana budi kufungua."

³⁷ "Nasimama, nabisha mlangoni, na kama mtu yeyote atafungua!" Mungu haufungui moyo wako, Yeye hubisha tu

nawe huna budi kuufungua. “Nasimama, nabisha, na kama mtu yeyote ataisikia Sauti Yangu, na kufungua, nitaingia na kula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.” Sasa, *kula* katika Agano la Kale, ama katika siku za mashariki za ziara ya Bwana duniani, kulikuwa, *kushirikiana*. “Nitaingia na nitaifanya ushirika pamoja naye, tuketi chini na kuzungumza mambo.” Hivi hutaki Yeye afanye hivyo pamoja nawe?

³⁸ Hapa Phoenix miaka michache iliyopita kulikuwako na mwanamume na mwanamke walioimba huo, nami ninao kwenye santuri ndogo ya raba, *Ningetaka Kulizungumzia Pamoja Naye*. Kesho sina budi kuhubiri kwenye kanisa hilo wanamotoka, nami natumaini wapo, ningetaka kuusikia tena.

³⁹ Ningetaka kusema, “Yesu, ulinipenda wakati njia yangu ilipofikia sana.” Wakati mzuri sana maishani mwangu ni wakati ambapo ningeweza kuketi chini, nayo njia yangu ikafikia, wala sikujua nielekee upande gani, mashariki, magharibi, kaskazini, ama kusini, na kuzungumza tu Naye. Ndipo muda si muda mwajua, nilikuwa upande ule mwingine wa hicho kitu. Kulizungumzia pamoja Naye.

⁴⁰ Mtu anapobisha mlangoni [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.], yeye anajaribu kuingia, anajaribu kuingia ndani. Anataka kuzungumza nawe, hiyo ndiyo sababu Yeye anabisha. Sasa, si jambo lisilo la kawaida kwa mtu kubisha mlango wa mtu fulani; tumekuwa nalo kote katika nyakati. Watu mashuhuri wamebisha milango.

⁴¹ Kwa mfano, vipi—kama tunganese usiku wa leo, vipi katika siku za Kaisari, yule mfalme mkuu wa Rumi, kama angeshuka kwenda kwenye nyumba ya mkulima mdogo, akabisha mlangoni [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.], naye huyo mkulima akakimbilia mlangoni, akafungua mlango, na hapo amesimama yule mfalme mkuu, mwenye nguvu wa Rumi akibisha mlangoni pake? Vema, maskini jamaa huyo mdogo karibu angeshikwa na mshtuko wa moyo. “Kuwazia ya kwamba Kaisari mkuu na mwenye nguvu amesimama mlangoni pangui!”

⁴² Ingekuwa ni heshima jinsi gani kwa mfalme mkuu wa Rumi kubisha kwenye nyumba ya mkulima mdogo! Mbona, angeweza, akitetemeka, kupiga magoti, naye angesema, “Bwana, kama kuna chochote ninachoweza, ambacho ningeweza kukufanyia, ewe mfalme mkuu, nitaifanya lolote unalotaka nifanye. Na kama inawezekana, iheshimu maskini nyumba yangu duni, kwa kuingiza miguu yako mlangoni. Itakuwa ni heshima kwamba nyumba yangu ilitembelewa na mfalme mkuu wa taifa hili kuu.” Na ingekuwa ni heshima.

⁴³ Ama huko Ujerumani, hayati dikteta, Adolf Hitler, katika siku za ukuu wake huko Ujerumani, kama angalienda mlangoni pa askari wa Kijerumani na kubisha mlangoni, basi maskini huyo askari angekimbia mlangoni, bila kujua ni

nani aliyekuwa akibisha, naye akafungua mlango, na, mbona, kama angekuwa amemwona huyo Adolf Hitler mkuu, yule kiongozi wa Ujerumani, amesimama pale, maskini askari huyo angalisimama miguu sawa, ampigie saluti ya Kijerumani huku midomo yake ikitetemeka na machozi yakitiririka mashavuni mwake, angesema, “Ewe Kiongozi wa Ujerumani, umeiheshimu nyumba yangu. Ingia. Unanifanya nijisikie vizuri sana kujua ya kwamba ungekuja mlangoni pangu. Ni heshima ambayo kila mtu hawezi kuwa nayo, kwako, ewe Hitler mkuu, kubisha mlangoni pangu, na kuja hapa kuniheshimu kwa uwepo wako.”

⁴⁴ Ama kama Rais Dwight Eisenhower, rais wetu mpendwa sana, kama angekuja hapa Phoenix kesho, na angekuja nyumbani mwa Mwanademokrati aliye bora sana huko Phoenix, ingekuwa ni heshima kwako, ingawa ungetofautiana naye katika siasa, hata hivyo yeye ni mtu mashuhuri, yeye ni rais wa Marekani yetu. Yeye ni mtu mheshimiwa, mmoja wa watu waheshimiwa sana, walioko katika taifa hili ni rais wetu mpendwa, Bw. Eisenhower.

⁴⁵ Hivi majuzi tu malkia wa Uingereza alifanya ziara hapa. Vipi kama angekuja Phoenix, na kushuka kwenda nyumbani kwako, na kubisha mlangoni, nawe ungefungua mlango na hapo alisimama malkia wa Uingereza mlangoni pako? Ingawa yeye hana mamlaka juu yako, wewe huko katika milki yake, lakini hata hivyo, ungeheshimika kuwa na malkia mkuu kuliko wote duniani amesimama mlangoni pako kukutembelea.

⁴⁶ Ungesema, “Ewe malkia, ingia nyumbani kwangu. Na kama kuna kitu chochote hapa ambacho unatafuta, loo, ingekuwa ni heshima kwangu kukupa wewe.”

⁴⁷ Hakika, yeye ni mwanamke mashuhuri. Mmojawapo wa malkia mashuhuri sana duniani siku hizi ni malkia wa Uingereza. Kama angalikuomba kitu fulani kidogo ulichopenda kwa moyo wako wote, bado ungalimpa. Ingekuwa ni heshima kwako kufanya hivyo, haidhuru ulikithamini jinsi gani, ulimpa malkia mkuu kuliko wote duniani.

⁴⁸ Unaona, inategemea umuhimu wa mtu aliye mlangoni pako. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani: Ni nani aliye muhimu zaidi kubisha mlangoni pako kuliko Yesu Kristo? Yuko wapi mtu aliye mkuu zaidi anayeweza kubisha mlangoni pako kuliko Yeye? Naye amebisha milango mingi kuliko wafalme wote waliowahi kuwako ulimwenguni, ama watakaopata kuwako, na amekataliwa kuliko yeyote aliyewahi kukataliwa. “Nasimama mlangoni, nabisha.” [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Mungu wa Utukufu!

⁴⁹ Sasa, labda, kama Bw. Eisenhower angebisha mlangoni pako, labda angekutaka umpigie kura, ama labda anaweza kuwa na kitu kingine cha kuchukua kutoka kwako, umfanyie fadhila fulani; malkia anaweza kuelewa kwamba una masalio fulani

ambayo unathamini, na—naye angetaka kitu hicho, anataka kuchukua kitu kutoka kwako.

⁵⁰ Lakini sivyo ilivyo kwa Yesu, anapobisha, anataka kukupa kitu fulani: Kitu kizuri kuliko vyote ambacho kingeweza kutolewa, hicho ni Uzima wa Milele. Hiyo ndiyo sababu ya kubisha Kwake. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Kwa nini mtu yeyote amkatae?

⁵¹ “Nasimama, na kubisha, na mtu yeyote akifungua, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, naye pamoja Nami.” Anataka kukuponya, anataka kukusamehe dhambi zako. Anataka kukufanyia jambo zuri, na hata hivyo watu wanamkataa zaidi ya vile wangemkataa Rais Eisenhower.

⁵² Sasa, ninataka kusema kitu kama hiki: Kama Rais Eisenhower angejiyenyekeza, ama malkia wa Uingereza, naye angekuja nyumbani kwako na kubisha mlangoni pako [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.], ungejivunia hilo kwa kila mtu, ungetaka kila mtu ajue ya kwamba rais amekuja nyumbani kwako. Na hata hivyo Yesu anaweza kubisha mlangoni, na tunaona aibu kumwambia mtu yeyote juu yake, kumwonea Bwana Yesu aibu anapobisha, na kujaribu kukupa kitu fulani.

⁵³ Chukua msimamo wa taifa, chukua msimamo wa Phoenix. Kama Rais Eisenhower, ama Bw. Nixon, makamu wetu mpendwa wa rais, angekuja Phoenix na kwenda kutembelea nyumba yako na kubisha mlangoni pako, ingekuwa kwenye habari za kimataifa, naye angesifiwa kwa kujinyenyekeza. Watu wote maskini katika ujirani wenu na kote nchini wangepurahia kujua ya kwamba mtu huyo mashuhuri alijinyenyekeza kuja mlangoni pako ama mlangoni pangu. Na hata hivyo, Yesu hubisha usiku baada ya usiku hata kwa wauza pombe haramu, makahaba, malaya, Naye anakataliwa mbali kama mlokole. Hukumu itakuwaje?

⁵⁴ Loo, huenda mkaniambia, “Hebu kidogo, Mhubiri, tayari nimemkubali Yesu moyoni mwangu.”

⁵⁵ Labda hivyo ndivyo tu ulivyofanya, ulimkubali moyoni mwako, lakini ulijua anapoingia moyoni mwako, amekaribishwa vipi baada ya Yeye kuingia?

⁵⁶ Kama nikija nyumbani kwako, na wewe, nikabisha mlangoni pako, nawe unipe mkono wa kuume wa ushirika na kuniambia niingie ndani, na kisha useme, “Wewe simama papo *hapo*. Usianze kuingilia mambo ya nyumba yangu.”

⁵⁷ Vema, hivyo ndivyo karibu watu wengine wanavyomkubali Yesu. Mnajua, kuna zaidi ya mlango mmoja wa kuingia moyoni. Kuna milango, vyumba vidogo, moyoni, hapo ndipo unapoishi, katika vyumba hivi vidogo. Halafu basi wakati... Vipi kama tungeangalia baadhi ya vyumba hivyo na kuona ni nini?

58 Sasa, wazia hilo, vipi kama ukija nyumbani kwangu, na ukabisha mlangoni, nami nije niufungue mlango, ningesema, “Ingia.” Nawe uingie, ningesema, “Sasa, angalia hapa, sitaki uingilie mambo ya nyumba yangu. Wewe simama papo *hapo* na uniambie unachotaka, lakini usianze kujipumbaza kote nyumbani mwangu.”

59 Usingejisikia kukaribishwa sana. Nisingejisikia kukaribishwa nyumbani kwako.

60 Kama ukinikaribisha ndani, ninatarajia useme, “Karibu, Ndugu Branham, nina furaha sana kuwa pamoja nawe! Nyumba ni yako, itwae, fanya utakalo.”

61 Loo, ningefanya vivyo hivyo tu. Niingie ndani, nivue viatu vyangu, nilale kitandani, niende kwenye friji, nijichukulie sambusa kubwa mno, nijilaze hapo na kula. Ningejisikia nyumbani. Hivyo ndivyo Yesu anavyotaka kufanya moyoni mwako, anataka kujisikia yuko nyumbani, lakini tumemfungia nje kwa mambo mengi.

62 “Sasa, Yesu, nitakwambia ni kwa nini nimekuruhusu kuingia mlangoni mwangu, sitaki kwenda kuzimuni, ninataka kuokolewa mwishoni mwa haya maisha. Unaweza kuingia mlangoni, lakini sasa, usianze kuingilia mambo.”

63 Unapoingia katika moyo wa mwanadamu, hebu tuliwazie hili, kwamba upande wa kulia kuna chumba kidogo, mlango mdogo, na huo ni mgumu hata watu wengi hawataki mtu yeyote auingilie huo, nao unaitwa, juu ya mlango huo, “Mlango wa maisha yangu ya kibinafsi.”

64 “Sasa, Yesu, nitakuruhusu uingie, lakini usianze kuingilia maisha yangu ya kibinafsi. Kama itanibidi kuachana na chama changu cha karata, kama itanibidi kuachana na ku—kundi la chumba cha kuchezea biliadi ambalo ninashirikiana nalo, kama inanibidi kuitwa wa mtindo wa kale kwa sababu sivuti sigara pamoja na wanawake wengine, kama itanibidi kuchoma kaptura zangu na siwezi kuzivaa kama wanawake wengine, Wewe kaa papo hapo, usinisumbue.”

65 Hivyo ndivyo Wakristo wengi wanavyomkubali Yesu. Asingekaribishwa moyoni mwako.

66 “Usikatize ninii yangu yoyote... Mimi hunywa bia kidogo ya kujiburudisha, wala sikutaki ujisumbue na hilo, ila tu ni—nitakuruhusu uingie kwa sababu sitaki kwenda kuzimuni.”

67 Sasa, hivyo ndivyo ulivyomkubali Yesu? Yesu hataki kuingia namna hiyo. Wakati anapobisha moyoni pako [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.], anapoingia Yeye anataka kuwa Bwana wako. *Bwana* ni utawala. Yeye huingia moyoni mwako, akijua ya kwamba aliufanya moyo huo kwa ajili Yake. Unaweza kuchukua sehemu nyingine zote za mwili, bali moyo ndio mnara wa kuongozea, Naye anataka kuja kwenye moyo huu,

ili aweze kukuongoza, awe Bwana. Unamtaka kama Mwokozi wako, bali si Bwana wako.

68 Watu wengi sana husema, “Loo, ninamtaka kama Mwokozi wangu, nimemkubali kama Mwokozi wangu.”

69 Hilo ni jema, lakini je, umemkubali Yeye kama Bwana wako, akutawale, kukutawala, kukuongoza, aingie kwenye mlango huo wa maisha yako ya kibinafsi na kusafisha hicho chumba, achukue Damu Yake Mwenyewe na kuipaka kwenye hizo kuta?

70 Halafu moja kwa moja karibu na huo ni mlango mwingine mdogo unaoitwa, “Kiburi.” Loo, huo ni wa kutisha sana! Kila mtu anataka kiburi kidogo. Kama huwezi kumruhusu Yesu aingie na kukitawala kiburi, basi Yesu hatakaa, atatoka moja kwa moja. Kama unafikiri wewe ni bora kuliko akina Jones, ati unaendesha gari bora zaidi, ama unakula mlo bora zaidi, unavaa nguo bora kuliko akina Jones, nawe unajivuna, basi Yesu ataondoka kwenye moyo huo akipitia mlango ule ule alioingilia.

71 Loo, siku hii ya mambo makubwa ya ajabu-ajabu! Nina furaha kwa ajili ya watu walio nao, na njia, ambayo ni moyo ulosalimishwa, hata Yesu anaweza kuingia na kuwa Bwana, na Mungu, na Mwokozi, na Mtawala. Unapomwingiza Yesu moyoni mwako, majivuno hayo yote yatatoweka.

72 Nitakwambia kile itakachokufanyia, ubatizo mzuri wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu utafanya aliyevaa ovaroli na aliyevaa suti rasmi wakumbatiane, waitane ndugu; utafanya aliyevaa vazi la kaniki na aliyevaa hariri wakumbatiane, na kusema, “Dada!” Hivyo ndivyo Yesu anavyofanya wakati Yeye ni Bwana, lakini Yeye ni Mwokozi tu, vema, hilo halitoshi. Kama Yeye ni Mwokozi, hana budi kuwa Bwana pia apate kukuongoza kwenye wokovu Wake kama Yeye ni Mwokozi.

73 Kuna mlango mwingine mdogo pembeni tu, ni mlango wa imani. Loo, ipo mingi. Hebu tuzungumze juu ya imani kwa muda kidogo tu.

74 “Sasa, Yesu, nitakuruhusu uingie, bali nina imani yangu mwenyewe.”

75 Vema, Yeye hawezi kukufanyia mengi kama una imani yako mwenyewe. Sitaki imani yoyote, nataka imani Yake. Imani yangu haifai kitu, imani ya Mungu ndiyo tunayohitaji, imani ya Mungu ndani yetu. Imani yangu haifai chochote, imani yako haifai chochote, inahitaji Kristo kuingia na kusimama katika mlango huo wa imani na kuwa Bwana, Bwana juu ya imani yako.

76 Unaposoma katika Biblia, “Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Imani yako itasema, “Hilo haliwezekani.”

Lakini imani Yake itasema, “Amina, Mimi ndimi.”

77 Kama mkosoaji akisema, “Siku za miujiza zimepita.”

Imani ya Mungu itasema, “Hajui anachozungumzia.”

⁷⁸ Kama mkosoaji akisema, “Yesu haponyi.”

Roho Mtakatifu akisimama katika mlango wa imani yako atasema, “Mimi ndimi Bwana niponyaye magonjwa yako yote.”

⁷⁹ Inaleta tofauti sana kumwalika kwenye mlango huo wa imani. Mwajua, Maandiko tuliyokuwa tukiyasoma muda mfupi uliopita yalisema ya kwamba “Uko uchi, na ni mwenye mashaka, wewe ni maskini, mnyonge na kipofu, wala hujui.” Hiyo ndiyo hali ambayo kanisa litafikia, uchi.

⁸⁰ Je, waweza kuwazia mtu barabarani akiwa uchi, wala hajui? Kama mtu huyo anajua hilo, atajifanyia msaada, ama mwanamke mtaani, ama mtu ambaye hajavaa nguo. Na kama wakijua ya kwamba wako hivyo, watajaribu kujipa msaada, lakini kisa cha kusikitisha: wamerukwa na akili sana hawajui.

⁸¹ Na siku hizi, watu wanaotembea kwenye barabara za miji hii wako uchi mbele za Mungu wala hawajui. Hiyo ndiyo sehemu ya kusikitisha. Wanajaribu kujifunika kwa kanuni fulani za imani za kanisa, kama vile Hawa alivyofanya katika bustani ya Edeni, majani ya mtini ya kujitengenezea. Mungu anahitaji kifuniko cha Damu iliyomwagika. “Nakushauri ununue nguo nyeupe kufunika uchi wako.”

⁸² Halafu alisema, pia, “Wewe ni kipofu,” tukinena kiroho, “kipofu, nami nitakushauri ununue Kwangu dawa ya Macho.”

⁸³ Unajua, Mungu ana uponyaji kwa kila kitu, nafsi zilizo na ugonjwa wa dhambi, miili, waliorudi nyuma. Chochote ulicho, Mungu anayo tiba katika kabati Lake kubwa la dawa.

⁸⁴ Mwajua nilipokuwa mvulana mdogo, tuliishi huko chini katika, huko chini kabisa mashariki, kusini-mashariki mwa Kentucky kwenye Milima ya Cumberland. Na watu wangu, tuliishi katika kibanda kidogo cha magogo, kilikuwa na vyumba viwili, nacho kilikuwa ni kitu cha kusikitisha. Hawakuwa na sakafu yoyote ndani yake, ila udongo. Naye Baba alikuwa amekata kilele cha kisiki, karibu kinene *hivi*, akaweka miguu mitatu chini kikawa meza, kisha akapasua maskini kipande kimoja kutoka ghalani na kutengeneza be—benchi ndogo kusudi maskini hawa Branham wadogo wangeweza kuketi pale na kula chakula chao cha kutwa.

⁸⁵ Na kwa, kulikuwa na kitanda kimoja, na hicho kilikuwa ni cha Baba na Mama, kimeyekwa upande wa kushoto wa hiyo nyumba unapoingia kutokea jikoni. Nasi watoto ilitubidi kupanda ngazi, ngazi ya kujitengenezea, miti viwili michanga na vijiti vilivyoikingama, tulipanda juu darini na kulikuwa na godoro kuukuu la majani makavu. Sijui kama mumewahi kuona moja au la. Kitanda cha kale cha manyoya? Na walikuwa na viezeko vya mbao juu yake, na—navyo vili—viliwekwa kwenye mwanga wa mwezi, nao walikuwa wamevipindua juu. Nayoa

maskini hiyo mianya kwenye hayo magogo, Mama angetufunika sisi watoto kwa kipande cha turubai usiku, kwa maana theluji ikipuliza ndani ingetuambukiza mafua.

⁸⁶ Na wakati mwingine kama wavulana wadogo, tulikuwa tisa, jinsi tungeyumbayumba kutoka chini ya hicho kifuniko. Ndipo ingekuwa asubuhi, macho yetu yangefumbwa kabisa kutokana na baridi, Mama alisema yalikuwa na matongotongo, sijui ni kitu gani, bali yeye aliyaita *matongotongo*, yangeshikamana, yawe baridi machoni mwako.

⁸⁷ Babu alikuwa mwindaji, alitega mitego na kuwinda maishani mwake mwote, Nyanya alikuwa Mhindi, Mhindi wa Cherokee, nasi tulikuwa na kitibu-yote nyumbani mwetu, hiyo ilikuwa ni mafuta ya kuuni, rakuuni. Babu angewakamata, kisha angetoa mafuta, akayatia kwenye mkebe. Nayo yalikuwa mazuri kwa kifaduro, ama koo linalouma, ama—ama kidole kilichochubuliwa, chochote kile, karibu yalikuwa ni kitibu-yote nyumbani mwetu.

⁸⁸ Kwa hiyo wakati Mama alipokuja kwenye vipandio, nami nilikuwa ndiye kifungua mimba, basi angesema, “William, njoo huku chini.”

Ningemgeukia ndugu yangu, Edward, ambaye ametuacha sasa, nilimwita Humpy, nami nikasema, “Amka Humpy, Mama anaita.”

Kasema, “Siwezi kufungua macho yangu.”

Nikasema, “Wala mimi siwezi.”

⁸⁹ Nao hao wavulana wadogo wote karibu wasingeweza kufungua macho yao, kwa sababu hapo palipitia upepo baridi, tulikuwa tumetoka chini ya kifuniko, kinga, nasi tukashikwa na homa, pia tulikuwa na matongotongo machoni mwetu.

Mama akasema, “Hiyo ni sawa, Mpenzi, nitapanda juu katika dakika chache tu.”

⁹⁰ Naye angechukua mafuta ya kuuni na kuyaweka kwenye ji—jiko na kuyapasha moto vizuri. Nasi wenyewe tukala hiyo rakuni. Kwa hiyo basi, angeyachemsha kabisa mafuta haya ya kuuni, kisha apande juu, na kuyasugua macho yetu kwayo, mpaka matongotongo yote yakatoka. Amini usiamini, yeye alitusaidia nayo, tukawa sawa.

⁹¹ Hilo huenda likasaidia kufungua macho hapa kawaida, lakini tumekuwa na kipindi cha baridi, pia, Wakristo wengi wametoka chini ya kifuniko, chini ya ulinzi wa Bwana Yesu, kumekuwa na kipindi cha baridi kote nchini wakisema ya kwamba siku za miujiza zimepita, na ibada za uponyaji, na upuuzi huu wote wa Roho Mtakatifu, hauna chochote. Huenda ulinaswa kwenye huo ushawishi, umefunga macho yako kabisa kwa mambo ya Mungu.

⁹² Wakati Malaika wa Mungu atakapokuja huku katika siku za mwisho kuakisi Nuru ya kuja kwa Yesu, huenda usiweze kuliona. Nisingeagiza mafuta ya kuuni, bali ninajua kuna Dawa ya macho ambayo Mungu anayo, inaitwa Roho Mtakatifu, Mafuta ya Mungu yaliyotiwa mafuta kutoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, ambayo yatafungua macho yako, nawe utaweza kuona ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule leo kama alivyokuwa jana, na atakuwa milele.

⁹³ Roho Mtakatifu wa Mungu, siku hizi, akiingia kutoka kwenye ibada kuu za uponyaji, akishuka kwenye uhalisi, Yesu akija miongoni mwa watu na kufanya na kutenda ishara zile zile za kukaribia kwa mwisho wa wakati huu, kama alivyowafanyia Wayahudi wakati alipomwambia Filipo alikuwa chini ya mti, ama, Nathanaeli alikuwa chini ya mti wakati Filipo alipomwona.

⁹⁴ Naye akasema, “Rabi, ulinijuaje Wewe?” wakati alipomwambia alikuwa mtu mwaminifu, Mwisraeli, wala hana hila. Wakati Yesu alipomwambia mahali alipokuwa, alianguka miguuni Pake na kusema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli,” kwa sababu alikuwa ameufungua moyo wake kwa Roho wa Mungu akibisha, ambaye alikuwa ametabiriwa na Musa, kiongozi wao, akisema, “Bwana, Mungu wenu, atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi. Na itakuwa ya kwamba yeyote asiye msikia Nabii huyu atakatiliwa mbali.” Na karibu taifa zima lilikatiliwa mbali.

⁹⁵ Mungu alibisha. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Kanisa liliangalia, na kusema, “Unajua, mtu huyo ni mpiga ramli, Beelzebuli.”

⁹⁶ Yesu akasema, “Mkisema hivyo kunihusu Mimi, nitawasamehe, lakini siku moja, Roho Mtakatifu atakuja, na kusema neno moja dhidi Yake hakutasamehewa kamwe.” Hivi huoni kanisa linajikatilia mbali tena kwa kutoifungua moyo yao, na kumruhusu Roho Mtakatifu aingie?

⁹⁷ Hivi hakumwambia yule mwanamke kisimani, “Nenda kamwite mumeo”? Samaria haikuwa imemwona kamwe, bali walikuwa wakimtazamia.

Naye akasema, “Sina mume.”

Akasema, “Vema, umekuwa na watano, na yule unayeishi naye siye wako.”

Moyo wake ukafunguka, akasema, “Bwana, hapana shaka Wewe ni nabii. Tunajua Masihi yuja.”

⁹⁸ Loo, jamani! Mwanamke huyo alijua mengi zaidi kumhusu Mungu kuliko wahubiri wengi wajuavyo. Hiyo ni kweli. Ingawa katika sifa zake mbaya, alikuwa na moyo ambao ungeweza kufunguka wakati Mungu alipobisha mlangoni, alijua Maandiko Matakatifu, ya kwamba siku hiyo ilikuwa imekaribia.

⁹⁹ Akasema, “Ninajua ya kwamba yuaja Masihi, tunajua hilo, na atakapokuja, atafanya jambo hili.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹⁰⁰ Moja kwa moja akaingia moyoni mwake. Huko chini kote mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?”

¹⁰¹ Hivi Masihi yuyu huyu hakusema kabla tu Yeye hajarudi, kwamba ishara iliyopewa Sodoma na Gomora ingerudi tena katika wakati wa Mataifa?

¹⁰² Kristo anabisha moyoni. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] “Yeye yule jana, leo, na hata milele,” Neno Lake hulinena, Roho Wake hulithibitisha miongoni mwa watu. Kwa nini usiufungue moyo wako na kumruhusu aingie na awe Bwana? Yeye ni mwema sana kwetu, na hata hivyo, sisi ni katili sana Kwake.

¹⁰³ Tunayathamini makanisa yetu, wachungaji wetu, washiriki wetu wa kawaida, mashemasi wetu, ninii yetu, mashirika yote, tunawathamini, nao wanafanya kazi nzuri sana, wengi wao, Bwana ashukuriwe, lakini hata hivyo, inahitaji mtu binafsi.

¹⁰⁴ Kanisa haliwezi kuufungua moyo wako, inakubidi kuufungua moyo wako; kanisa haliwezi kuingia moyoni mwako, Yesu hana budi kuingia moyoni mwako; kanisa haliwezi kuwa Bwana juu yako, Kristo ni Bwana juu yako. Hata hivyo wewe ni mfuasi wa kanisa, hiyo ni jamii Yake, hiyo ndiyo njia Yake ya kufanya mambo, lakini hata hivyo, huna budi kumruhusu aingie, halafu ujiunge na waaminio wengine, hilo ndilo lifanyalo.

¹⁰⁵ Sasa, tunaishi katika siku za mwisho. Tunaangalia pande zote kuona wema wa Mungu. Jinsi ambavyo katika siku zetu wakati hakuna tumaini... Angalieni hapa, hivi mlitambua ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho? Je, mnatambua watu wote mashuhuri ulimwenguni wanabashiri ya kwamba jambo fulani...? Mbona, tunaweza kulipuliwa dakika yoyote! Naye Roho Mtakatifu katikati ya hayo amekupa majaliwa ya kuja katikati mahali alipo Yeye, na kubisha mlangoni mwa moyo wako. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] “Tazama, nasimama mlangoni, nabisha.”

¹⁰⁶ Unasema, “Ndugu Branham, siwezi kulielewa.”

Fungua tu mara moja. Acha aingie.

¹⁰⁷ “Sijui jinsi ya kuamini ishara hizi, na mambo haya yote, sijui.”

¹⁰⁸ Hivyo ndivyo yule Mkushi alivyomwambia Filipino, “Ninawezaje kujua jambo hili, mtu asiponifundisha?” Roho Mtakatifu alitumwa hapa kama mwalimu, hebu aingie moyoni mwako, atakufundisha ya kwamba Yesu ni yeye yule.

¹⁰⁹ Alisema, “Roho Mtakatifu atakapokuja, Yeye atanishuhudia Mimi.” Nasi tunajua ya kwamba hiyo ni kweli.

¹¹⁰ Sasa, Yeye ni mwema sana, inaonekana kana kwamba tungeweza kuuthamini wema Wake. Wakati ulimwengu unapokufa kwa njaa, tuna mengi. Ni watoto wangapi wadogo huko India usiku wa leo, na mahali pengi, wasio na chakula wangetoa chochote? Ni watu wangapi wenye njaa wanaomtafuta Mungu wangetoa chochote kuketi katika mkutano huu usiku wa leo?

¹¹¹ Hebu niwaonyeshe tamasha ambayo ni ya kusikitisha sana: Ni watu wangapi wamezama ng’ambo ya maeneo ya rehema wakaingia kuzimu ya ibilisi na mateso ya jinamizi? Jinsi wangependa kurudi na kupata nafasi moja zaidi! Wangepanya nini usiku wa leo kama Yesu angekuja kuzimuni na kubisha moyoni mwao?

¹¹² “Mkinikataa katika siku hii, katika siku za msiba wenu mtakapoita, nitacheka tu.” Hii ndiyo ile siku, usiahirishe kesho, leo ndiyo siku ya wokovu. Hata hivyo wengi wenu, labda, wamengojea kwa miaka mingi, Yeye amebisha, na kubisha, na kubisha, hujibu.

¹¹³ “Yeye ni Mungu mwema,” kama vile Oral Roberts amesema mara nyingi. Yeye ni Mungu mwema, Yeye ni Mungu wa rehema, na Yeye pia ni Mungu wa hukumu.

¹¹⁴ Sasa, huko chini Kusini ambako ninaenda sana, nilikuwa kwenye likizo ndogo hivi majuzi huko chini. Kundi la watu, la maskini watu duni kabisa huko chini Florida. Tulikuwa huko nje tukivua samaki, na hapo ndipo Ndugu Evans alipoumwa na yule nyoka mchacharisha, wala sikuwahi kumwona hapo kabla maishani mwangu, maili mbili huko nyuma, ingenibidi kumbeba mtu mwenye ratili mia moja na themanini.

¹¹⁵ Maskini mchacharisha wa ardhini mkubwa, mbaya kuliko yule wenu mwenye kupindapinda, wakati wowote, alimwuma mguuni, ndipo mguu wake wote ukapooza tu, akijaribu kunisaidia kumshisha baasi wa ratili kumi na mbili, kwenye magugu ambamo mamba, na kila kitu, wanavizia kote. Naye akaruka kumnyakua, ndipo akapiga mayowe tu na kuushika mguu wake. Nikatoka na kulikuwa na mashimo mawili ya meno namna *hiyo*, damu ikitoka ndani yake.

Akasema, “Ndugu Branham, upande wangu wote umeganda, unauma sana.”

¹¹⁶ Ningewezaje kumbeba kupitia kwenye hivyo vinamasi? Alikuwa na uzito wa yapata ratili mia moja na themanini, urefu wa futi sita. Ndugu yake alikuwa ameumwa miezi michache kabla ya hapo, mwenye dhambi, akaenda hospitalini akiwa hali mbaya sana.

Ndipo nikasema, “Loo, Ndugu Evans! Mungu mwenye rehema, kuwa . . .” Nikawazia, “Nifanyeje?”

¹¹⁷ Nikakumbuka yale Maandiko. Ilikuwa ni kitu gani? Mtu akibisha mlangoni. “Mimi ni Bwana, Mungu wako, mimi ni msaada unaonekana tele wakati wa shida.” Nikakumbuka Yeye alisema, “Watavikanyaga vichwa vya nyoka na nge, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.”

¹¹⁸ Nikaweka mkono wangu juu ya mguu wake, huku akipiga mayowe, machozi yakidondoka kutoka mashavuni mwake namna hiyo kutokana na maumivu, Nikasema, “Baba wa Mbinguni, ninabisha mlangoni Pako, tuko katika hali ya hatari. Uturehemu, Ee Mungu!”

¹¹⁹ Basi wakati tukisema hivyo, nami nikanukuu Maandiko, niliangalia juu naye alikuwa akicheka, maumivu yote yalikuwa yamekwisha. Tukavua samaki siku nzima. Ndipo usiku huo saa sita, tulipokuwa kule chini tukipiga picha, nadhani ilikuwa mahali fulani karibu na pale, Gene, kuwafanya watalii wote waje kuona msururu huu mkubwa wa baasi ambao Bwana alikuwa ametupa, ndipo ndugu yake akaja nasi tukaisimulia hiyo hadithi.

¹²⁰ Ndipo ndugu yake mwenye dhambi akasema, “Ngoja kidogo, Welch,” kasema, “ni sawa kuwa wa kidini, bali si mwendawazimu.” Akasema, “Unajua, nililala hospitalini miezi mitatu, na miezi miwili baadaye nimefungwa kalibu mguuni mwangu na huko, huko kuumwa mara moja na mchacharisha.” Kasema, “Nenda ukapate msaada wa kimatibabu, upesi tu uwezavyo.”

¹²¹ Akasema, “Angalia hapa, ndugu, huenda unajua mambo mengi, bali hujui mambo yote. Kama Mungu wangu angeweza kunikomboa kutoka saa tano asubuhi ya leo mpaka saa tano, usiku, anaweza kunishughulikia muda uliosalia.”

¹²² Ilikuwa ni kitu gani? [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Akibisha mlangoni Pake katika wakati wa dharura. Haitupasi kungojea mpaka wakati huo wa dharura. Siku moja mauti yatakuja mlangoni pako [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani.], nayo yatabisha. Loo, jamani, utatamani kubisha huko wakati huo!

¹²³ Nimewaona watu waliomcheka Roho Mtakatifu, nimewashikilia walipokufa. Usimcheke Kristo, mheshimu, mheshimu. Achaneni na theolojia zenu zote na hisi zenu. Acheni tu Roho Mtakatifu. . . Ulipewa hisi tano, lakini hizo hisi tano, akili zako, kamwe hukupewa zikakuongoze. Ile hisi ya sita, ambayo ni imani, ulipewa ikakuongoze, hiyo ni ile hisi ya sita, hiyo ndiyo ile hisi kuu, inakuongoza.

¹²⁴ Huko chini Shreveport, Louisiana, pamoja na maskini rafiki yangu msiri, Ndugu Moore, kulikuwa na maskini ndugu mweusi kule chini ambaye, alikuwa ni mzee mzuri, jina lake lilikuwa Gabrieli. Walimpa, mama yake, mwanamke wa kidini, baba

yake, walimpa jina la *Gabrieli*, lakini sote tulimwita *Gabe*, kwa ufupi tu.

¹²⁵ Naye mke wake alikuwa Mkristo hodari, mtu wa kupendeza sana, naye mchungaji wa kanisa alikuwa ni ndugu mzuri sana, nao walifanya yote waliyoweza kumfanya mzee Gabe apate kunyoshwa na Mungu. Lakini Gabe alipenda kurusha dadu, na—na yeye—yeye kamwe asingejiweka sawa na Mungu.

¹²⁶ Basi Gabe alipenda kuwinda, na vivyo hivyo na mchungaji, naye mchungaji angekuja, na kumchukua Gabe na kumpeleka mawindoni, na—na kadhalika. Basi siku moja walipokuwa wakiwinda, maskini Gabe alikuwa amelemewa sana na mzigo wa wanyama pori, ndege na sungura, hata ilikuwa vigumu kwake kuwabeba, hata alikuwa amewawekelea juu ya mtutu wa bunduki yake, wakija, wote ambao angeweza kukokota ndani.

¹²⁷ Nao walikuwa wakija kuzunguka maskini kijia fulani, basi mzee Gabe akaendelea kutazama nyuma kuelekea magharibi, nalo jua lilikuwa linazama. Miaka yake ilikuwa inasonga, miaka yake ya hamsini. Naye akaendelea kuliangalia jua hilo.

¹²⁸ Mchungaji, kwa uaminifu, akienda zake njiani, wote wawili wakiwa na wanyama wengi sana. Baada ya kitambo kidogo, mchungaji alihisi mkono begani mwake ukimgusa. Kasema, “Mchungaji?” Naye akageuka. Gabe alikuwa akimtazama, machozi yakitiririka mashavuni mwake. Akageuka tena na kutazama kuelekea jua, akageuka na kusema, “Mchungaji, asubuhi, kwa kuwa ni Jumapili asubuhi, *Mimi* kuja kanisani pamoja na mke wangu mpendwa. *Mimi taenda* kwenye benchi ya *wambolezaji* na kufanya maungamo yangu. Halafu nitajitafutia kiti karibu tu na upande wa mbele niwezavyo kupata, hapo nibaki mpaka Yesu atakapokuja kunichukua. Nitaishi mwaminifu kwa Mungu tangu leo na kuendelea.”

¹²⁹ Mchungaji akageuka na kumkumbatia ndugu yake, kasema, “Gabe, nakutakia heri, jamani.”

¹³⁰ Kasema, “Unaona jua hilo likitua kule, Mchungaji? Jua langu linatua, pia. Basi Kitu fulani kilibisha moyoni mwangu dakika chache tu zilizopita.”

¹³¹ Akasema, “Ni mahubiri gani niliyohubiri, Gabe? Ni ujumbe gani niliohubiri ukasikia, uliokufanya ubadilike? Au waimbaji waliimba wimbo gani uliokufanya ubadilike na kumpa Bwana Yesu maisha yako?”

¹³² Akasema, “Mchungaji, nimekusikia ukihubiri mahubiri mazuri sana mara nyingi, nimesikia kwaya zikiimba mpaka ilionekana kana kwamba walikuwa na nyimbo za Malaika,” akasema, “zote zilikuwa nzuri sana,” akasema, “lakini hizo sizo zilizosababisha hilo, Mchungaji, kwa jumla.” Kasema, “Nilikuwa nikija huku nikiwazia jinsi alivyo mwema kwangu, jinsi tu alivyo mwema.”

¹³³ Akasema, “Unajua, Mchungaji, mimi sina shabaha,” akasema, “nisingeweza kupiga risasi chochote. Nasi tulikuwa na haja ya chakula nyumbani mwetu, basi angalia wanyama hawa wote ambao Yeye amenipa. Hakika, lazima ananipenda, la sivyo asingenifanyia hivyo.” Akasema, “Niligeuka kusema, ‘Asante.’ Ndipo Kitu fulani kikabisha moyoni mwangu, na kusema, ‘Jua la maisha yako linatua.’”

¹³⁴ Yeye ni mwema kwetu. Gabe alifanya yale tu aliyomwambia mchungaji angefanya, na kadiri nijuavyo mimi angali ni mshiriki mwanzilishi wa kundi hilo la Kipentekoste huko chini. Kwa sababu aliangalia huko nje na kuuona wema wa Mungu, ndipo Kitu fulani kikabisha moyoni mwake, na kusema, “Gabe, nilikupa hivyo vitu, usingeweza kupiga chochote risasi, nilikupa wewe.”

¹³⁵ Ninataka kukuuliza usiku wa leo: “Ni nani aliyekupa motokaa yako? Ni nani aliyekupa kile chakula kizuri ulichokula usiku wa leo? Ni nani aliyekupa nguo hizi nzuri ulizovaa?” Unawezaje kumkataa, wakati jua la ustaarabu linapotua, jua la wakati linatua? Yesu yuaja, Naye anabisha usiku baada ya usiku kwenye milango ya moyo. Hivi hutafungua usiku wa leo, maskini rafiki yangu, aliyeunjika moyo, na kumwacha aingie ndani yako, na kula pamoja nawe, nawe pamoja Naye? Hivi hutawazia hilo sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu?

¹³⁶ Ninaomba ya kwamba mtakuwa na kicho sana sasa. Huenda Roho Mtakatifu akapata mahali Pake katika mioyo. Yeye ni mwema jinsi gani kwako? Angalia waliolala hapa hospitalini; angalia vile ulivyookoka na kifo muda mfupi uliopita katika gari hilo; wazia juu ya wakati ulipomwambia mtoto huyo, ama mama huyo, “Nitakutana nawe ng’ambo ya bahari, kule, mama, baba, mume, mke, ndugu, mtoto.” Na hata hivyo Yeye amekubariki, nawe unaweza kuwa hapa usiku wa leo, hilo linatoka kwa Mungu.

¹³⁷ Huku mmeinamisha vichwa vyenu, sijui kama mtu fulani hapa usiku wa leo katika kusanyiko hili linaloonekana angetaka kumwambia Yesu, “Bwana, umekuwa mwema sana kwangu, ninakutaka uingie moyoni mwangu moja kwa moja usiku wa leo. Usiache kupambazuke asubuhi bila Wewe kuingia moyoni mwangu. Ninataka kulizungumzia pamoja Nawe. Ninajua tuko katika wakati wa mwisho, sayansi yetu inasema ndiko tuliko, taifa letu linajua ndiko tuliko, jeshi la wanamaji linajua ndiko tuliko, jeshi la nchi kavu linajua ndivyo, na zaidi ya hayo yote, Biblia inasema ndiko tuliko, naye Roho Mtakatifu, pamoja na ishara Zake kupitia Kanisa anathibitisha kwamba ndiko tuliko. Umekuwa mwema sana kwangu, Bwana, ningependa kuzungumza Nawe kabla sijavuka.”

¹³⁸ Je, ungetaka kumwinulia mkono wako kwa ajili ya ushirika

mdogo kabla hatujafunga kwa maombi? Inua tu mkono wako, useme, “Mungu, unirehemu, ninataka kuzungumza na Wewe.” Bwana akubariki. Bwana akubariki, mama. Bwana akubariki. Juu kwenye roshani, upande wa kulia, Bwana akubariki hapo, bwana.

¹³⁹ Mtu mwingine? “Ningependa kulizungumzia. Unabisha, Bwana, Ninataka ku—ninataka kuzungumza na Wewe kidogo tu dakika chache zijazo. Ndugu Branham, nijumishe katika maombi yako.”

¹⁴⁰ Mungu atayasikia maombi yako.

¹⁴¹ Roshani upande wa kushoto, mtu fulani inua mkono wako na kusema, “Niombee, Ndugu Branham.”

¹⁴² Roshani mbele, Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Chini hapo, sakafuni, Mungu akubariki upande wangu wa kulia. Hilo ni zuri. Loo, ninaona mikono yenu yote nyuma hapo ndani, wote upande wa kulia, Mungu awabariki. Mungu ambariki kila mmoja wenu.

¹⁴³ Safu ya katikati kupitia hapa, inua mkono wako, useme, “Unirehemu, Bwana. Ni—ninataka kulizungumzia kabla sijaondoka hapa. Unabisha moyoni mwangu, Na—najisikia kama ninapaswa kulizungumzia na Wewe, nina mambo fulani ningetaka kutatua.”

¹⁴⁴ Mtainua mikono yenu, marefu ya katikati? Marefu ya upande wa kushoto, mwaweza kuinua mikono yenu? Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, wewe, na wewe, na wewe. Mungu awabariki. Hilo ni jema. Mungu aturehemu.

¹⁴⁵ Wewe ni Mungu wa vizazi vyote. Nawe umesema ya kwamba katika siku hizi za kanisa la Laodikia, ya kwamba Wewe ungesimama mlangoni na kubisha, na kama mtu yeyote angesikia hiyo hodi na angefungua mlango, Wewe ungeingia, na kula pamoja nao.

¹⁴⁶ Sasa kumekuwako na wengi sana hapa, na labda thelathini au zaidi usiku wa leo wameinua mikono yao, tukijua ya kwamba Wewe uko hapa ukibisha mlangoni mwao. Sasa, Bwana, uliahidi ya kwamba ungeingia, ninakuamini Wewe, wanakuamini Wewe, kwa hiyo nena amani mioyoni mwao, Bwana. Nami natoa ombi hili kwa niaba yao: kwamba hakutakuwako na mmoja wao atakayepotea, jalia wote waokolewe kwa neema Yako ya ajabu. Yesu na aingie mioyoni mwao usiku wa leo, ashike hatamu, na milango yote iwe wazi, apate kuwa Mwokozi na Bwana pia, apate kuwaongoza kupitia kwenye mitego ya mashimo yenye moshi na kuwaongoza kwenye:

Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa
chini ya hiyo gharika,

Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

¹⁴⁷ Na kutoka hapo hadi kwenye Makao makuu ya Mungu aliye hai ambako nafsi haifi kamwe, ambapo hakuna maradhi, huzuni, wala uzee, hakuna mauti huko yanayoweza kuingia mahali hapo patakatifu, pa raha. Bwana, jalia nafsi yao ipate raha yake ya Milele tangu saa hii na kuendelea juu ya ahadi hiyo kuu. “Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu. Naye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe. Nitamfufua katika siku ya mwisho, nimpe Uzima wa Milele.” Na tena, imeandikwa, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna,” wakati uliopo, “Uzima wa Milele, hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi mikononi Mwako sasa.

¹⁴⁸ Wabariki wale walio wagonjwa na wanaoteseka. Jalia hawa walioinua mikono yao kesho asubuhi, kama vile mzee Gabe huko Louisiana, alivyopata njia yake kwenda kanisani, huko akabatizwa katika imani ya Kikristo, akamkiri Yesu kama Mwokozi wake, akachukua mahali pake upande wa mbele, na kubaki huko, jalia wafanye vivyo hivyo, Bwana. Nisipoweza kuwapa mikono katika maisha haya, jalia katika Uzima huo ujao, jalia nishiriki pamoja nao katika nyakati zote, katika Umilele.

¹⁴⁹ Wabariki wale walio wahitaji hapa usiku wa leo, Baba. Kama kuna wengine waliosalia kutoka jana jioni ambao hawakuponywa, tunaomba ya kwamba utawaponya usiku wa leo. Nena nao kwa njia ya rehema wapate kujua ya kwamba ni Roho Wako anayebisha mlangoni pao. Jalia wakukaribishe usiku wa leo, Bwana. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
gharika hiyo,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.
Hupoteza madoa yao yote ya hatia,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia;
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
gharika hiyo,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

¹⁵⁰ Loo, hivi hamumpendi? Yeye si ni wa ajabu, mwema sana, amejaa sana rehema na wema? Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Yeye alivyo mwema! Hebu sote tuwe na roho ya kuabudu sasa, tuimbe ubeti hu—huu:

Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahia kuona
Chemchemi hiyo katika siku zake;
Hapo naomba, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshwe dhambi zangu zote.

151 Hebu na tuuimbe sasa. Vema, Ndugu Creech, sawa.

Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahia kuona
Chemchemi hiyo katika siku zake;
Na hapo naomba, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshwe dhambi zangu zote.
Nioshwe dhambi zangu zote,
Nioshwe dhambi zangu zote;
Na hapo naomba, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshwe dhambi zangu zote.

152 Loo, hivi hamuupendi huo utamu mzuri wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu? Loo, jamani! Loo, ninapenda tu hilo! Hebu na tuimbe, "Amani! Amani! Amani ya ajabu, ikishuka kutoka kwa Baba juu." Mnaujua? Vema.

Amani! Amani! Amani ya ajabu,
Inayoshuka chini kutoka juu kwa Baba;
Pitia rohoni mwangu milele, naomba,
Katika mawimbi yasiyopimika ya upendo.

. . . Amani ya ajabu,
Inayoshuka chini kutoka juu kwa Baba;
Pitia rohoni mwangu milele, naomba,
Katika mawimbi yasiyopimika ya upendo.

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Kwani alinipenda kwanza . . .

153 Hebu tuahidi uaminifu wetu huku tumeinua mikono yetu.

Kamwe sitamwacha,
Kamwe sitamwacha,
Kamwe sitamwacha,
Kwani alinipenda kwanza.

154 Ee Bwana, Yehova mkuu, jinsi tunavyokupenda usiku wa leo, kwa sababu Wewe ulitupenda kwanza, na ulitupenda sana tulipokuwa wenye dhambi hata ukamtoa Mwanao wa pekee, ili kila amwaminiye awe na Uzima wa Milele. "Hili tunalojua, tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, tunapokuwa na ushirika sisi kwa sisi na kupendana. Nayo Damu ya Yesu, Mwanao, inatusafisha na udhalimu wote."

155 Baba, jalia Roho Mtakatifu, wimbi baada ya wimbi, apitie nafsini mwetu na kutusafisha na mambo ya ulimwengu. Ingia mioyoni mwetu usiku wa leo, Bwana, na sio tu kuwa Mwokozi, bali uwe Bwana. Chukua mawazo yetu na uyatupe mbali nasi, Bwana, yakiwa ni kinyume na Neno Lako. Hebu tumwone Yesu pekee na Yeye amesulubiwa. Jalia tuenende si kulingana na mwongozo wa nia zetu, bali kwa uongozi wa Roho Mtakatifu. Tujalie, Baba.

¹⁵⁶ Takasa kundi hili la watu usiku wa leo ambalo limekuwa likiketi hapa, jalia kamwe wasisahau milango iliyo ndani ya mioyo yao. Sasa jalia Roho Mtakatifu aje na kujifunua Mwenyewe kwetu. Mungu, kama tulipata neema machoni Pako, jalia aje sasa na kuthibitisha ya kwamba Wewe uko hapa pamoja nasi katika siku hii ya mwisho.

¹⁵⁷ Wewe ndiwe Mlango wa zizi la kondoo, Wewe ndiye Mfalme ajaye, Wewe ni Bwana wa Utukufu, Mungu wa Ibrahimu, Ua la Uwandani, Yungiyungi la Bondeni, Nyota ya Asubuhi, Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho, Yeye Aliyekuwako, na Aliyeko, na Atakayekuja, Shina na Mzao wa Daudi. Ee Mungu, Wewe ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, Wewe ni Mwokozi, Mponyaji, Wewe ni *Yote*, Bwana.

¹⁵⁸ Tunakupenda, na tunakuthamini, na tunafungua moyo wetu wote, Bwana. Jalia Mfalme wa Utukufu aingie. “Inueni enyi malango ya milele, mkainuke, na Mfalme wa Utukufu apate kuingia,” akimiliki kikamilifu kama Mwokozi, kama Bwana, kama Mfalme, kama Kiongozi, kama Gavana, kama Mpaji wa Amani, kama Kiongozi wa mapito yetu. Tujalie, Bwana. Tunaomba, katika Jina lake Yeye aliyetufundisha sisi sote kuomba hivi:

Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako
Litukuzwe.

Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike
duniani, kama huko Mbinguni.

Utupe leo riziki yetu ya kila siku.

Na utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi
tuwasameheavyo wanaotukosea.

Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule
mwovu:

Sasa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na
utukufu, hata milele. Amina.

¹⁵⁹ Wema wa Bwana u pamoja nasi. Loo, afadhali niwe hapa katika mkutano kama huu, pamoja na ushirika wa Roho Mtakatifu, tukiketi pamoja katika Ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu! Loo, ushirika wa furaha ya kiungu, hakuna kitu kama hicho chini ya mbingu.

¹⁶⁰ Yesu alisema, “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao. Kazi nizifanyazo Mimi, hao nao watazifanya; zaidi ya hizi, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele.”

¹⁶¹ Kuna mgonjwa yeyote jengoni? Inueni mikono yenu wanaotaka kukumbukwa katika maombi. Ni kila mahali tu. Ni wagonjwa wangapi walio hapa ndani, wanaojua ya

kwamba siwajui? Inua mkono wako. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Mungu anakujua? Inua mkono wako.

¹⁶² Kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye ataiheshimu Injili ninayohubiri. Kama Yeye si Mungu, kama amekufa, anabaki amekufa, Yeye yuko kaburini kama Waislamu wanavyosema, “Hebu tumwone akifanya jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa duniani na kuahidi atafanya, tungeamini Yeye alifufuka katika wafu. Lakini mafundisho yenu si zaidi ya yetu, nasi tunaweza kutoa saikolojia kadiri mnavyoweza.”

¹⁶³ Loo, hawatambui ya kwamba Yesu wetu mwenye upendo yu hai. Kila ahadi aliyotoa ni ya kweli, kila kitu alichofanya. Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Kama wewe ni mgonjwa, mguse Yeye, Atatenda vile vile tu alivyotenda alipokuwa hapa duniani.

¹⁶⁴ Yule mwanamke aligusa vazi Lake, akaenda, na kuketi chini, ama popote alipoenda katika umati, Yeye aligeuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

¹⁶⁵ Ndipo Petro akasema, “Vema, wote walikugusa,” akamkemea. “Kwa nini useme jambo kama hilo?”

¹⁶⁶ Akasema, “Lakini nimekuwa dhaifu, nguvu zilinitoka. Mtu fulani alinigusa Mimi.” Ndipo akaangalia kote mpaka akamwona, akamwambia kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma, imani yake ilikuwa imemwoko, naye akaponywa.

¹⁶⁷ Kama Yeye ni Yesu yeye yule, nawe unaweza kumgusa kwa imani, hakuna vazi hapa kwako kugusa, bali kuna Mungu unayeweza kumgusa kwa imani yako, kwa kidole chako cha imani, kidole cha Mungu kilicho ndani yako, hebu kiguse, ndipo Yeye atafanya kazi kupitia matawi Yake, Yeye ni Mzabibu. Hana midomo ila yetu, hana macho ila yetu ya kutenda kazi hapa duniani. Roho Wake Mtakatifu yuko hapa kuyatia nguvu matawi Yake kufanya kazi ile ile.

¹⁶⁸ Kama jamaa fulani alitoa tikitimaji kutoka kwenye mmea, na mtu mwingine akarudi na kupata boga, haikutokana na mmea ule ule. Kama ulitoa, ilipandikizwa kibandia, bali kama mmea huo ukipata kuzaa mmea mwingine, utakuwa na tikitimaji.

¹⁶⁹ Kwa hiyo kama mzabibu wa kwanza uliotoka kwenye hilo Tawi, ulikuwa na Kanisa la Kipentekoste lililofanya ishara zile zile ambazo Yesu alifanya, tawi linalofuata litafanya jambo lile lile. Tumepandikiza miti, hakika, tukaweka balungi kwenye mchungwa, nafikiri utazaa, naam, bali si tunda la asili. Mti huo kamwe haukuzaa hayo, ulipandikizwa. Tuna vipandikizi vingi kupita kiasi siku hizi. Ninataka Roho yeye yule aliyekuwa juu Yake.

170 Niliwahubiria kuhusu Ibrahimu na kuthibitishwa kwa lile agano, wakati alipolipasua agano hilo, halina budi kuumana vivyo hivyo. Yeye yule... Mungu alipofanya agano Lake na mwanadamu pale Kalvari, Yeye alirarua sehemu ya Mwanawe Mwenyewe, akautwaa mwili Wake juu, na kuuinua kutoka kaburini, na kuuweka kwenye mkono Wake wa kuume, akamtuma Roho aliyekuwa katika mwili huo arudi Kanisani. Kanisa hilo itabidi liwe na Roho wa namna ile ile Mwilini mwake ambaye mwili huo ulikuwa naye, la sivyo hilo agano si sahihi. Loo, ni hakikisho la jinsi gani, hakikisho lililobarikiwa!

Ombeni sasa.

171 Kama Roho Mtakatifu atakuja na angalau awachukue watu wawili au watatu hapa usiku wa leo, tulichukua kadi zetu za maombi jana usiku, na kama Yeye atakuja usiku wa leo na kufanya kama tu alivyofanya alipokuwa hapa duniani...

172 Ni wangapi wanaojua ya kwamba vile alivyothibitisha huduma Yake ya kuwa Masihi, ilikuwa ni kujua siri ya moyo wao? Hiyo ni kweli kabisa, hakika. Waaminio waliokusudiwa Uzima wa Milele waliliamini. Kulikuwako na wengi pale waliokiri kuwa waaminio ambao hawakukusudiwa Uzima wa Milele. Si ni jambo la kuhuzunisha kuona ya kwamba watu, wanadamu, wataketi na kutazama, na hata hivyo hawawezi kuliona?

173 Yesu alisema, "Vema, Isaya alisema vema juu yenu: Mna macho wala hamwezi kuona, masikio wala hamwezi kusikia." Mnaona? Hata hivyo wakiliangalia moja kwa moja. Loo, kamwe wasingeweza kuelewa hilo, kwa sababu hawakukusudiwa Uzima wa Milele.

174 Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu." Mnaona?

175 Loo, hivi hamna furaha kwamba ninyi ni kondoo, usiku wa leo? Hivi hamna furaha mnaweza kuona Neno Lake likidhihirishwa, kuona kuja kwa Bwana Yesu?

176 Vema, ninyi ombeni sasa. Roho Mtakatifu na anisaidie. Sasa, hili halitakuponya, bali litakufanya ujue... Angalia jinsi... Sio katika kona fulani yenye giza, papa hapa nje ambapo unatazama, kama Bwana wetu alivyokuwa.

177 Kabisa hatufahamiani, siwajui, si zaidi ya vile Yesu alivyomjua Petro wakati alipokuja, ama hao wengine, ama chochote kile, Alimjua. Na mwisho kabisa, ilifichwa kwao kwa muda mrefu, ndipo wakasema, hatimaye, "Loo, sasa, sasa tunaamini. Sasa tunajua ya kwamba Mungu hukuonyesha mambo yote."

178 Kwa sababu Yeye alisema, "Siwezi kufanya lolote, mpaka nitakapomwona Baba akilitenda." Ni yeye yule jana, leo... Ila tu si mwili Wake. Damu Yake huitakasa miili yenu na mwili

wangu, kusudi Roho Wake aweze kuingia na kuendeleza kazi mpaka ukomo. Hiyo ni kweli.

Ombeni, aminini.

¹⁷⁹ Ili tu mpate kujua, nitaugauza mgongo wangu kuelekea kusanyiko hili. Sasa kumbukeni, ninapofanya jambo hili, msiache nipate barua zinazosema, “Ndugu Branham, ulijiita Malaika huyo.”

¹⁸⁰ Hilo ni kosa. Mimi ni mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema ya Kristo. Haidhuru nilifanya nini, haidhuru Mungu alinitia mafuta kiasi gani, kama hukutiwa mafuta pia, isingefanya kazi, imani yako ndiyo inayofanya jambo hilo. Hii ni karama tu, kuvuta tu wenzu nyuma vya kutosha kumwacha William Branham atoke jukwaani kusudi Yesu Kristo aweze kutenda kazi. Sasa hebu vuta wenzu wako nyuma vya kutosha hata unaweza kutoka jukwaani na Yesu Kristo anaweza kufanya kazi.

¹⁸¹ Nami ninawaambia, wakati hao...Roho wa Uzima anapoanza kupigana na roho wa mauti, jambo fulani linatukia. Giza haliwezi kukaa katika nuru, wala mauti hayawezi kukaa mahali penye uhai. Jambo fulani linatukia, likiwekewa msingi juu ya nini? Imani yako.

¹⁸² Nitageuza mgongo wangu upate kujua ya kwamba Neno la Yesu...Wakati yule Malaika aliposhuka kule Sodoma na akaenda kwenye...Sasa kumbukeni, mnaweza kuiona leo? Kundi la wasomi hawaipokei. Hata haijatumwa kwao. Iko wapi? Kundi lililoitwa litoke, kundi lililoteuliwa.

¹⁸³ Hapo ndipo ilipokuwa kwenye kundi la Ibrahimu, lililoitwa litoke, likatengwa. Kulikuwako na waaminio, Lutu na kundi lake kule chini, kulikuwako na wasioamini, na wahudumu wawili, Malaika wahudumu walishuka kule wakiwa na Roho wa Mungu ndani yao na kuwahubiria, wakawaita watoke, “Tokeni kwake!” Lakini hawangesikiliza, ni wachache tu waliotoka.

¹⁸⁴ Ndivyo ilivyo sasa. Lakini yule Malaika aliyebacki nyuma ambaye alizungumza na Ibrahimu, Mteule, angalia alitoa ishara ya namna gani.

¹⁸⁵ Kasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Alijuaje alikuwa na...alikuwa na mke? Tena alijuaje jina lake lilikuwa Sara?

Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

¹⁸⁶ Akasema, “Nitakujilia, Ibrahimu.” Mwanadamu, akila nyama ya ndama, ugali, akinywa maziwa, kasema, “Kwa muhula wake, nawe utampata mtoto yule niliyekuahidi miaka ishirini na mitano iliyopita.”

¹⁸⁷ Naye Sara, akiwa na karibu miaka mia moja, tisini, na Ibrahimu mia moja, alicheka moyoni mwake, kwa namna fulani, “*Ha-humph!*”

Akasema, “Kwa nini Sara akacheke?”

¹⁸⁸ Yesu alisema hiyo itarudi tena, huyo atakuwa ni Roho Mtakatifu aliyekuwa katika Mwanadamu, “Roho Mtakatifu yeye yule atarudi katika mwili wa Kanisa Langu kwenye wakati wa mwisho na kuonyesha ishara ile ile. Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

¹⁸⁹ Angalia kundi lililolijia, angalia kundi lililoipokea. Wangesema nini huko Sodoma juu ya kitu kama hicho? Mnaona? Mungu anajua mahali pa kuipeleka.

¹⁹⁰ Ombeni sasa. Bwana wa Mbinguni na awasaidie. Kote tu jengoni, ninyi ombeni tu. Fungua moyo wako. Iweni kimya kabisa, kaeni kimya, iweni na kicho.

¹⁹¹ Ninamwona mwanamke, mwenye wasiwasi sana, ambaye anaomba. Siwezi kutambua mahali alipo. Kidogo tu mpaka nipapate. Naam, ameketi papa hapa chini. Huyu mama upande huu wake, anayeniangalia, ana ugonjwa wa moyo; ana shida ya mishipa. Kama unaamini kwa moyo wako wote, nyote wawili wekeaneni mikono hapo na kuamini kwa moyo wenu wote. Papo hapo, hiyo ni kweli, uh-huh, vema. Mungu alijibu maombi. Nyote wawili mmeponywa sasa, mnaweza kwenda nyumbani, mpate afya.

¹⁹² Yeye si ni wa ajabu? Sasa waligusa nini? Siwajui hao wanawake. Kama hiyo ni kweli, inueni mikono yenu, enyi akina mama, kama siwajui. Hiyo ni kweli, vema. Lakini Mungu anawajua.

¹⁹³ Sasa ngojeni, kuna mtu nyuma yangu, anayeomba. Ni mwanamume, ana ugonjwa wa figo, yeye, na matatizo mengi sana, amefungwa gango. Bw. Balrich, kama unaamini kwa moyo wako wote! Sikujui, sivyo, bwana? Hunijui mimi, lakini yaliyosemwa ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mikono yako. Vema, umeponywa sasa, imani yako imekuponya.

Sasa mnaamini? Iweni na imani.

¹⁹⁴ Yupo mama aliyeketi papa hapa nje akiniangalia, akiomba. Nuru hiyo iko juu yake, ile Nuru iliyowaongoza wana wa Israeli, ile Nguzo ya Moto iliyodhihirishwa katika mwili, kasema, “Nilitoka kwa Mungu, kisha nikaenda, naenda kwa Mungu.”

¹⁹⁵ Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Sauli wa Tarso, akienda zake huko chini Dameski, aliangukwa chini na Nuru iliyoyapofusha macho yake. Kwa muda alikuwa kipofu. Nuru iyo hiyo ilikuwa ni Yesu Kristo, ambaye ni Nuru ya ulimwengu. “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

¹⁹⁶ Huyu mwanamke hajiombe mwenyewe, bali anamwomba mwanamume, ana ugonjwa wa moyo na hajaokoka. Anaishi katika mji huu, lakini huyu mwanamke anatoka mji mwingine, anatoka Tucson. Unaamini kwa moyo wako wote ataponywa?

Kama unaamini, inua mkono wako. Sikujui, sivyo, mama? Sijawahi kukuona maishani mwangu. Hilo ndilo ulilokuwa ukiombea. Je, hilo ndilo ombi lako? Kama ndivyo, punga mkono wako namna *hii*.

Je, unaamini kwa moyo wako wote? Mwaminini Mungu.

¹⁹⁷ Huyo mvulana wa Kihindi aliyeketi hapo mwisho, Mungu awe pamoja nawe, ndugu yangu. Sikujui, lakini bila shaka ninakuheshimu. Unataka Mungu awaponye watoto wawili wagonjwa. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini Yeye atafanya hivyo? Unaamini ya kwamba atafanya hivyo? Mama yako ameketi moja kwa moja chini yako hapo mbali kidogo, labda hiyo itakufanya uelewe ninachozungumzia. Unaamini Mungu anaweza kuniambia mama yako ana shida gani? Ana ugonjwa wa mapafu. Mungu akubariki, Mmarekani halisi.

¹⁹⁸ Kulikuwa na mtu aliyeketi papa hapa, akamwangukia Mhindi huyo na kumheshimu sana, ameketi chini mstarini hapo. Ana mtoto anayemwombee, huyo mtoto amefanyiwa upasuaji kwenye mshipa fulani wa ubongo, mshipa wa uwiano, ama kitu fulani. Hiyo ni kweli, bwana, kutoka California. Ninaamini Bw. Works, ama Weerts. Amini, huyo mtoto atakuwa mzima.

¹⁹⁹ Unaamini? Wewe uliyeinua mkono wako, ulisema unaamini, je, unaamini? Mara tu uliposema hivyo, kitu fulani kiliugusa moyo wako. Ulikuwa na ugonjwa wa moyo, umekwisha. Huishi hapa, unatoka kaskazini mwa hapa, unatoka kwenye mji unaoitwa Globe. Sikujui, lakini hiyo ni kweli.

²⁰⁰ Kuna jamaa mdogo aliyeketi huko nyuma ambaye anaugua pumu, karibu amekwisha, yabisi kavu pia, jina lake ni Jordan.

²⁰¹ Unamwamini Bwana wangu? Anapobisha moyoni mwako, unaamini Yeye yupo hapa? Sasa, kama unaamini Yeye yupo hapa, kwa nini usinitii kama mtumishi Wake? Wekeaneni mikono kama ninyi ni waaminio. Mnaona yale Maandiko yasemayo? Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa, wewe mwombee yule uliyemwekea mikono yako, usijiombee mwenyewe.

²⁰² Na, maskini mama aliyeketi hapa chini kutoka Chicago, ambaye amesumbuliwa sana, na amekoma hedhi, na unasumbuliwa na mirija, kuwa na imani sasa, utapona. Usiogope tena. Nenda nyumbani na ushangilie, kwa sababu unaenda kupona huo. Hiyo hapo Nuru ya Mungu ikining'inia juu yako, halina budi kutukia! Usiwe na shaka, amini.

²⁰³ Kila mmoja wenu, mahali pote pamejaa Roho Mtakatifu sasa hivi. Malaika wa Bwana, ishara aliyotoa, mlango wa mioyo yenu unabishwa. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] "Mimi ni Bwana, Mungu wako, nikuponyaye magonjwa yako yote. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Wakiweka

mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Omba kwa njia yako mwenyewe.

²⁰⁴ Mwenyezi Mungu, Mwanzilishi wa Uzima, Mpaji wa kila karama njema, ninasimama kama mtumishi Wako kuwatangazia watu hawa Injili Yako, kwamba ibilisi anawadanganya, Yesu Kristo amewaponya.

²⁰⁵ Toka, Shetani! Ninakukemea katika Jina la Yesu Kristo. Waache hawa watu, wapate kwenda na kuponywa!

²⁰⁶ Haya basi. Nguvu za Mungu za uponyaji ziko juu yenu. Fanyeni nayo yale yanayoonekana ni mazuri kufanya. Nguvu kuu za Mungu za uponyaji ziko pamoja nanyi sasa, ni zenu kudai. Furahini katika Bwana. Simameni kwa miguu yenu. Sijali umelemaa kiasi gani, simama. Mwamini Bwana Yesu Kristo, unaweza kupata ulichoomba. 

60-0312 Mlango Wa Kuingia Moyoni
Madison Square Garden
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org